## Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki ipo wapi?


Milima ya Tao la Mashariki inapatikana katika wilaya 14 katika mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Dodoma na Iringa kama ifuatavyo:

- Pare Kusini na Kaskazini iliyopo katika wilaya ya Same na Mwanga
- Usambara Magharibi na Mashariki iliyopo katika wilaya ya Muheza, Lushoto na Korogwe
- Nguu iliyopo katika wilaya ya Kilindi
- Nguru iliyopo katika wilaya ya Mvomero
- Uluguru iliyopo katika wilaya ya Morogoro na Mvomero
- Ukaguru iliyopo katika wilaya ya Kilosa
- Rubeho iliyopo katika wilaya ya Mpwapwa na Kilosa
- Malundwe iliyopo katika wilaya ya Morogoro
- Udzungwa iliyopo katika wilaya ya Kilombero, Mufindi na Kilolo
- Mahenge iliyopo katika wilaya ya Ulanga

(Kwa maelezo zaidi tazama ramani)

## Eneo limehifadhiwa kwa kiasi gani?

Kiasi cha asilimia 15 sawa na Kilometa za mraba 5400 za eneo la Milima ya Tao la Mashariki imefunikwa na Misitu yenye unyevu. Maeneo yanayolindwa kama vile misitu ya hifadhi, mbuga za wanyama za Taifa na hifadhi za asili ni asilimia 25 sawa na kilometa za mraba 7400 za eneo lote la Milima ya Tao la Mashariki. Maeneo madogo madogo ya misitu yanayolindwa na vijiji ni kama vile vipande vya misitu ya asili, misitu ya ukoo na maeneo ya makaburi.
Makazi ya asili mengi yaliyobaki katika Tao la Mashariki, hasa misitu ipo katika maeneo haya yaliyohifadhiwa, hata hivyo uwezo wa kipesa kwa ajili ya kusimamia maeneo hayo ni mdogo.



## Ramani ya Milima ya Tao la Mashariki




## Ofisi za Mradi zipo wapi?

Ofisi za Mradi zipo Morogoro Mjini. Ofisi zilizokuwa za maliasili Mkoa.

## Kwa maelezo zaidi wasiliana na :


Mratibu wa Mradi,
Uhifadhi na Usimamizi wa Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki
S.L.P 289, Morogoro
Simu: 023 3082
Simu pepe: 023 3084
Barua pepe: easternarc@easternarc.or.tz

au

Mkurugenzi Mtendaji,
Mfuko wa Hifadhi ya Milima ya Tao la Mashariki,
S.L.P 6053,
Morogoro, Tanzania.
Simu: 023 3660
Simu pepe: 023 3113
Barua Pepe:
eamcef@easternarc.or.tz

'Conserving Biodiversity for Sustainable Development'
EASTERN ARC MOUNTAINS CONSERVATION ENDOWMENT FUND
EAMCEF
MFUKO WA HIFADHI YA MILIMA YA TAO LA MASHARIKI

# Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki - Chanzo cha Maji na Umeme kwa Taifa




**Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki inatoa maji kwa mikoa minne Tanzania na kwa ajili ya kutengeneza zaidi ya asilimia 50 ya umeme unaotengenezwa nchini**

## Ni ipi hiyo?

Milima ya Tao la Mashariki ni Mlolongo wa Milima ya kale inayoanzia kusini mwa nchi ya Kenya mpaka Kusini mwa nchi ya Tanzania. Misitu iliyomo kwenye Milima ya Tao la Masharik imekuwepo kwa zaidi ya miaka 30 milioni.

**Nishati ya Umeme inayotumia maji kutoka Misitu ya Tao la Mashariki inachangia asilimia 50 ya nishati ya umeme wa taifa.**

## Kwa nini ni ya Muhimu?

Zaidi ya watu milioni tano wanakaa na wanategemea milima hii kimaisha. Pamoja na kupanda mazao mengi ya chakula kwa ajili ya mahitaji yao vilevile kuna kiwango kikubwa cha matunda na mboga zinazozalishwa na kuuzwa katika miji mbalimbali. Hali hii imetokana na kuwa na hali ya hewa na mandhari nzuri katika misitu iliyo katika milima hii. Kuna aina nyingi za mimea na wanyama ambao wanapatikana katika misitu hii pekee na si mahala pengine popote duniani. Inasemekana zaidi ya aina za wanyama 100 na mimea 800 wanapatikana katika misitu ya milima hii. Aina nyingi za viumbe hawa hai wamo katika hatari ya kutoweka na hupatikana katika maeneo madogo (vipande) yaliyobaki ya msitu. Milima ya Tao la Mashariki inajulikana kimataifa kama moja kati ya maeneo 25 duniani yenye bioanuai ya hali ya juu inayohitaji kutunzwa.

Milima ya Tao la Mashariki ni vyanzo vya maji kwa miji ya Dar es Salaam, Tanga, Iringa na Morogoro

## Shughuli za utunzaji ni zipi?

Zaidi ya asilimia 70 za misitu ya asili ya Milima ya Tao la Mashariki imeharibiwa vibaya. Eneo kubwa limebadilishwa na kuwa la kilimo katika kipindi cha miaka 200 iliyopita. Upanuzi wa maeneo kwa ajili ya kilimo bado ni tatizo kubwa kwa kuzingatia maisha ya muda mrefu ya misitu na wanyama waliyomo.

Matatizo mengine ni kama:

- Moto kichaa
- Uvunaji usio endelevu wa mbao na kuni
- Uchimbaji wa madini kama dhahabu na vito.
- Uwindaji usio endelevu (haramu) hasa wa wanyama wakubwa



Mkondo wa mto uliopo kwenye msitu umeharibiwa kwa sababu ya uchimbaji ya dhahabu

## Mradi wa Uhifadhi na Usimamizi wa Misitu ya Milima ya Tao la Masharik (CMEAMF)

Mradi wa Uhifadhi na Usimamizi wa Misitu ya Milima ya Tao la Masharik (CMEAMF) ni ushirikiano kati ya Idara za serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO), Wizara ya Mali asili na Utalii - Idara ya Misitu na Nyuki ndio wenye wajibu mkubwa katika mradi huu unaofadhiliwa na Mfuko wa Kimataifa wa mazingira (GEF). Mradi umegawanyika katika makundi mawili: Mkakati wa Tao la Msharik na Milima ya Uluguru, na una uhusiano wa karibu na Mfuko wa hifadhi wa Milima ya Tao la Masharik.

### Mradi wa CMEAMF una lengo kubwa moja

**"Kukuza na kutekeleza mkakati ya uhifadhi itakayo hakikisha uhifadhi endelevu wa Milima ya Tao la Masharik, kwa ajili ya kuhifadhi misitu na bioanuwai, uhakika wa maisha kwa zaidi ya watu milioni waishio kwenye milima hii na wanaotegemea maji na umeme kutoka maeneo haya"**

## Mkakati wa Tao la Masharik

Mradi unawajibu wa kutengeneza mikakati wa kuhifadhi Tao la Masharik itakayo jumuisha mambo yafuatayo;

- **Elimu:** Mpango wa elimu kwa mapana utakaowapa wadau habari katika kufanya maamuzi ya jinsi ya kutumia rasilimali za misitu. Mkakati huu umejumuisha Habari, Elimu na Mawasiliano unatengenezwa na Kikundi cha Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG).
- **Kuboresha utunzaji** wa misitu ya hifadhi katika Milima ya Tao la Masharik na utambuzi wa misitu ya hifadhi kama maeneo yanayotumiwa kwa kuhifadhi bioanuwai.
- **Ufadhili endelevu** kwa ajili ya kutunza mitandao ya hifadhi na kukuza maisha ya Jamii zinazoishi jirani na misitu na kusaidia mradi wa EAMCEF
- **Ufuatiliaji** wa rasilimali za misitu, bioanuwai na huduma ya maji na umeme kwa jamii. CARE inawajibika katika kutengeneza mkakati wa maendeleo ya kiuchumi kwa jamii.

Mkakati wa Tao la Masharik unafanya kazi kwa kushirikiana na wilaya na vyama vya kiraia vya maendeleo ya wananchi vinavyozunguka Milima ya Tao la Masharik.

## Milima ya Uluguru



Milima ya Uluguru ni moja kati ya milima yenye umuhimu mkubwa wa maji na bioanuwai kati ya milima yote iliyomo katika Tao la Masharik. Milima hii ni chanzo cha maji kwa miji ya Dar es salaam na Morogoro, vilevile ni kati ya maeneo matatu muhimu kwenye Tao hii kwa kutunza bioanuwai na rasilimali za misitu zilizo katika hatari ya kutoweka.

Kitengo cha milima ya Uluguru (UMADEP) kina lengo la kujaribu mawazo na njia za kuhakikisha uhifadhi endelevu hasa katika misitu iliyo jirani na makazi ya watu. Kitengo kinatoa eneo la majaribio kwa mkakati wa uhifadhi wa Tao la Masharik. Kitengo hiki cha Uluguru kinaongozwa na CARE kwa kushirikiana na TFCG, WCST, na UMADEP

## Mfuko wa Hifadhi wa Milima ya Tao la Masharik (EAMCEF)

EAMCEF ni mpango wa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania, Benki ya Dunia na Mfuko wa Mazingira wa Dunia. Mfuko huu unadhumuni la kusaidia uhifadhi endelevu wa shughuli zinazohusiana na kuendeleza bioanuwai na kuboresha kazi za ekolojia katika maeneo yenye kipaumbele kwenye Milima ya Tao la Masharik. Mfuko huu unaendeshwa na bodi ya wadhamini na inafanya kazi si kwa kutengeneza faida kama shirika lisilo la kiserikali. Shughuli zote zinaratibiwa na ofisi ya mfuko wa hifadhi.

Tanzania Forest Conservation Group

UNDP

care

Global Environment Facility